WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA

SHULE YA SEKONDARI ISMANI
S.L.P. 378,
IRINGA.
18/12/2020

Simu : 0753-825-060 Mkuu wa Shule
0752-161-569 M/Mkuu wa shule

Kumb. Na. ISS/MK/US/VOL/ 01

JINA LA MWANAFUNZI _____
S.L.P _____
IRINGA.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ISMANI WILAYA IRINGA MKOA WA IRINGA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

1. **UTANGULIZI**
   Ninayo furaha kubwa kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari Ismani mwaka 2021. Shule ya Sekondari Ismani ipo umbali wa km 48 kaskazini mashariki mwa mji wa Iringa katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa. Usafiri wa basi kutoka Iringa mjini unapatikana stendi ya zamani ya mabasi ya mkoa wa Iringa nauli ya Tsh 2000.
2. **KUFUNGUA SHULE**
   Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021 saa 1:30 asubuhi. Kila mmoja lazima awepo wakati huo na kuitika Jina lake. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 25/01/2021 (ndani ya siku 14). Ukichelewa hutapokelewa bila ya kibali kutoka kwa afisa Elimu Mkoa.
3. **KUSAJILIWA RASMI**
   Kila mwanafunzi lazima ahakikishe kuwa amesajiliwa katika daftari maalumu la usajiri na kupewa namba ya usajili baada ya kukamilisha taratibu zote za usajili. Usipokamilisha maelezo haya HUTASAJILIWA.
4. **UNAPOKUJA SHULENI;**
   Uje na barua hii pamoja na fomu zilizoambatanishwa zikiwa **zimejazwa kikamilifu.**
   Fomu hizo ni;
   (a) Fomu ya mwanafunzi na mzazi kukubali nafasi ya kujiunga kidato cha kwanza.
   (b) Fomu ya kupimwa afya na **daktari** wa Serikali.
5. **MIHULA YA SHULE**
   Shule ina mihula miwili yaani:
   - ✓ Muhula wa kwanza Januari hadi Juni.
   - ✓ Muhula wa pili Julai hadi Desemba.
6. **MAHITAJI YA SHULE**
   - Ndoo moja ya ujazo wa lita 10 kwa ajiri ya utunzaji wa mazingira.
   - **Ream moja** ya karatasi za photocopy A_4 kwa mwaka.
   - Fagio moja ya kukaushia maji (dryer)

- **Mafaili** mawili (spring file ya plastic) kwa ajiri ya kutunzia kumbukumbu za mwanafunzi
- Fagio mbili ya kufagilia mazingira ya shule (**CHELEWA)**.
- **Jembe** moja lenye mpini kwa wasichana na **kwanja** moja kwa wavulana.

7. SARE YA SHULE

WAVULANA

i. Suruali mbili rangi damu ya mzee (kitambaa kizito)
ii. Shati mbili nyeupe mikono mifupi.
iii. Suruali iwe pana yenye marinda manne ya kuvalia kiunoni.
iv. Viatu vyeusi vya kamba na kung'arishwa kwa kiwi (jozi mbili na kuendelea)
v. Soksi nyeupe ziwe ndefu (jozi mbili na kuendelea)
vi. Mavazi ya michezo (T-shirt(**Jezi**) 02 za bluu,bukta 02 za bluu na raba 01)
vii. **T-shirt ya shule rangi ya dark blue inapatikana shuleni kwa sh.10,000**
viii. Sweta rangi ya damu ya mzee (ifanane na suruali) iliokolezwa shingo V
ix. Mkanda mweusi upana usizidi inchi $1\frac{1}{2}$.
x. Tai rangi ya damu ya mzee.

WASICHANA.

i. Sketi mbili rangi ya damu ya mzee mshono wa rinda box isiyo bana (kitambaa kizito) yenye urefu mpaka kiwiko cha miguu.
ii. Shati mbili nyeupe mikono mifupi.
iii. Skafu ya rangi ya damu ya mzee .
iv. Viatu vyeusi vya kamba na kung'arishwa kwa kiwi (jozi mbili na kuendelea)
v. Soksi nyeupe ziwe ndefu (jozi mbili)
vi. Sweta rangi ya damu ya mzee (ifanane na sketi) iliyokolezwa shingo V.
vii. Mavazi ya michezo (T-shirt(**Jezi**) 02 za bluu ,bukta 02 za bluu ,skin tight 01 na raba 01)
viii. **T-shirt ya shule rangi ya dark blue inapatikana shuleni kwa sh. 10,000**
ix. Rangi ya ijabu ifanane na shati la shule (kwa wale wanaohusika tu)
x. Mahitaiji mengine ya mtoto wa kike.

8. MAHITAJI YA MWANAFUNZI ANAYEISHI KATIKA DAHALIA (HOSTELI) YA SHULE

i. Ndoo ya kuhifadhia maji (lita 20)
ii. Shuka jozi mbili (rangi ya pink na blue)
iii. Blanketi moja
iv. Chandarua chenye dawa futi $2\frac{1}{2}$
v. Vifaa vya kutosha vya usafi wa faragha
vi. Taulo
vii. Vyombo vya kulia chakula
viii. Shamba dress gauni rangi ya dark blue.
ix. Traki moja ya dark blue (sweta na suruali yake)
x. Bima ya Afya Sh. 10,000 kwa wanafunzi wa hosteli tu.

9. MAHITAJI MENGINE MUHIMU YA MWANAFUNZI

i. Kalamu za kutosha.
ii. Daftari kubwa 09 (Kaunta book) na daftari ndogo 09 (Msomi).
iii. Mkebe wa hesabu.
iv. Tochi moja ya betri au ya sola itakayotumika kukiwa na tatizo la mwanga.

10. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII (ZITEKELEZWE NA MWANAFUNZI)

Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

a) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana ratiba ya shule ni lazima,
b) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation),

c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa hapa shuleni,
d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii,
e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule,
f) Kuvaa sale ya shule wakati wote unapotakiwa,
g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
h) Kutunza Mali za umma.

11. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE MWANAFUNZI.

a) Wizi.
b) Uasherati na ushoga.
c) Ubakaji.
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa Bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga,lugha ya matusi.
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g) Kuoa au kuolewa.
h) Kutoa mimba.
i) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
j) Kukataa adhabu kwa makusudi.
k) Kuwa na simu ya mkononi au laini ya simu.

Tabia njema ni ya lazima na inatiliwa mkazo hapa shuleni. Mwanafunzi mwenye tabia mbaya hafai kupewa elimu ya sekondari au hata elimu ya juu. Ni lazima mwanafunzi awe na tabia nzuri na kufuata taratibu za shule pia kuwatii wafanyakazi na walimu wengine wenye mamlaka. Heshima na adabu kwa mtu yeyote ni kitu cha lazima.

Unatakiwa kuvaa sare za shule kwa mshono uliokubaliwa na kwa wakati kama taratibu za shule zinavyoelekeza hasa;

a) Wakati wa masomo darasani
b) Wakati wa masomo ya jioni (remedial time na preparation time)
c) Safari zote za nje ya shule kwa jina la shule
d) Wakati wa kwenda hospitali
e) Wakati wa maandamano ya amani

Kwa usikivu na utulivu wa kitaaluma na kwa usalama wa kimalezi kwa mwanafunzi **SIMU ZA MKONONI HAZIRUHUSIWI SHULENI**, na mawasiliano yote yanayohusu malezi ya mwanafunzi ni kati ya mzazi/mlezi na utawala wa shule ana kwa ana au kwa simu ya shule namba **0744004215.**

Mwisho kabisa natumia nafasi hii tena kukukaribisha sana hapa Ismani Sekondari na ni matarajio yangu kuwa ufikapo hapa utaitumia vema fursa hii muhimu uliyotunukiwa na Taifa lako kwani wengi wameikosa.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.

……
MWASOMOLA C
MKUU WA SHULE

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
SHULE YA SEKONDARI ISMANI

FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA KIDATO CHA KWANZA.

Sehemu ya kwanza ya fomu hii ijazwe na mwanafunzi na sehemu ya pili ijazwe na Mzazi/Mlezi

SEHEMU YA KWANZA
(Sehemu hii ijazwe na Mwanafunzi mwenyewe)

WEKA PICHA YA MWANAFUNZI HAPA

Mimi ---------- (Mwanafunzi) kwa hiari yangu nakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na kidato cha Kwanza katika Shule Sekondari Ismani. Aidha naahidi kutoshiriki/kuanzisha migomo, fujo na makosa ya jinai.

Jina la Mwanafunzi ----------

Saini ya Mwanafunzi----------

Tarehe ----/------/20---

SEHEMU YA PILI
(Sehemu hii ijazwe na Mzazi/Mlezi)

Mimi ---------- Mzazi/Mlezi wa ----------
Nakubali/Sikubali nafasi aliyopewa mtoto wangu na kwamba muda WOTE awapo shuleni atalazimika kuwa mtii kwa Walimu, Wazazi, Viongozi na Jamii kwa ujumla. Atalazimika kufuata sheria zote za shule. Naahidi kuwa mwanangu atazifuata taratibu zote za shule hadi atakapo maliza shule.

Jina la Mzazi/ Mlezi ----------

Saini ----------

Tarehe ---/---/20---

HABARI ZA MZAZI/ MLEZI
(Fomu hii ijazwe na Mzazi /Mlezi)

1. Jina kamili la baba----------
2. Uraia ----------
3. Kazi yake ----------
4. Jina kamili la mama ----------
5. Uraia ----------
6. Kazi yake ----------
7. (Jina kamili la mlezi (iwapo haishi na wazazi wake) ----------

   kazi na anuani ya mzazi/mlezi ----------
8. Mtoto anaishi na Baba tu, Mama tu, Wazazi wote au Mlezi (kata yasiyohusika).
9. Dini ya mzazi/mlezi----------
10. Dhehebu ----------
11. Anuani kamili ya sehemu ambako mtoto atakuwa anakwenda wakati wa likizo---------
12. Mimi ---------- Mzazi/Mlezi wa taarifa hiyo hapo juu ni sahihi. Naahidi kushirikiana na walimu ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi, na mwenye bidii.

---------- ----------
Tarehe Saini ya Mzazi/Mlezi

MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY
ISMANI SECONDARY SCHOOL
MEDICAL EXAMINATION FORM
(To be completed by medical officer in respect of all new students)

Full name ----------

Age ----------

1. Blood count (red and white) ----------
2. Urine examination ----------
3. Stool examination ----------
4. Syphilis ----------
5. T.B Test ----------
6. Ear test ----------
7. Eye test ----------
8. Spleen ----------
9. Abdomen ----------
10. Additional information or any other Physical, Mental, Hereditary of infectious diseases

    ---

    Treatment after examination

MEDICAL CERTIFICATE

I certificate that the above concerned has been examined and found fit into pursue for further education.

Signature ----------

Designation ----------

Station ----------

(Official stamp)

Date ---/----/20---

NB: Fomu hii ijazwe na mganga katika hospitali inayotambulika na serikali baada ya kumpima mwanafunzi.